JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI.
SHULE YA SEKONDARI ITONA,

S.L.P 414, MAFINGA.
TAR: 10/12/2020.

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE: 0754-404414/0785777003
MAKAMU MKUU WAS HULE: 0753101885
KUMB.NA.ED/ITSS/S.3704/VOL.111/03

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITONA WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 na unatakiwa kuripoti tarehe 11.01.2021. jumatatu saa 1:00 asubuhi. Shule ya sekondari Itona ipo wilaya mufindi, tarafa ya Ifwagi, kata ya Ifwagi,katika kijiji cha Itona kilometa 30 kutoka mji wa Mafinga.

Shule ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wanafunzi wavulana na wasichana, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne.Kauli mbiu yetu ni **"EDUCATION IS LIGHT"**(ELIMU NI NURU) Huduma ya Hostel ipo(ya mtu binafsi) **kwa wasichana** inatolewa kwa wanafunzi wote wanaohitaji. Masomo yanayofundishwa ni **Uraia, Kiswahili, Kiingereza, historia, jiografia, fizikia, kemia, baiolojia, hisabati na Somo la literature in English** ambalo hufundiswa kuanzia kidato cha tatu.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YA SHULE:

WAVULANA.

- Suruali ya rangi ya damu ya mzee(dark red) moja na suruali ya rangi ya dark blue moja
- Mashati meupe mawili mikono mirefu
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili. Viatu viwe vyenye kamba.
- Tai moja ya Rangi ya bluu iliyokolea (dark blue)
- Soksi nyeusi pea 2
- Sweta 2:Moja ya damu ya mzee(dark red) lenye mshono wa V kifuani lisilo na maandishi ya pili bluu iliyokolea (Dark blue) yenye mshono wa V kifuani
- Bukta nyeusi na fulana rangi ya blue za michezo
- Raba za michezo
- Mkanda mweusi

WASICHANA.

- Sketi ya rangi ya damu yam zee(dark red)moja (1) na sketi ya rangi ya dark blue moja (1)
- Blauzi nyeupe mbili mikono mirefu
- Tai moja ya rangi ya blue iliyokolea (dark blue)
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili. Skuna na viatu vyenye kisigino kirefu havirususiwi. Viatu viwe vyenye kamba.
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Sweta 2:Moja ya damu ya mzee(dark red) yenye mshono wa V kifuani lisilo na maandishi nay a pili blue iliyokolea(dark blue)yenye mshono wa V KIFUANI
- Track suti nyeusi na tisheti ya rangi ya blue

Kwa wale watakao vaa hijabu ni lazima rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule mfano ingeweza kuwa nyeupe kama blauzi.

*MUHIMU:*Zingatia sampuli ya vitambaa iliyoambatanishwa kwenye fomu hii.

MAHITAJI MENGINE YA SHULE.

- Madaftari 20, kumi counter book za masomo ya darasani na kumi daftari za kawaida kwaajili ya mazoezi na majaribio ya kila wiki. Kila somo litakuwa na daftari lake maalumu la mazoezi na majaribio.
- Begi la mgongoni dogo jeusi kwa ajili ya kuwekea daftari na vifaa vingine vya masomo
- Kamusi (Dictionary) ya kiingereza- kingereza.
- Mkebe wa hesabu mmoja (mathematical set 1)
- Mahitaji ya chakula cha mchana debe moja la mahindi,lita tano za maharage na shilingi elfu kumi ya viungo,kukoboa mahindi na kumlipa mpishi kwa miezi sita(KAMATI YA WAZAZI INARATIBU)
- Vifaa vya kufanyia usafi ndoo ya kita kumi,jembe na fagio.

NB. Ukaguzi wa sare na vifaa utafanyika ili kuhakikisha kila mwanafunzi ana sare na vifaa alivyoagizwa.

03.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana na elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika Appendix(kiambata) **A, B na C.**

KARIBU SANA ITONA SEKONDARI

.....

MLOWE.D.E

MKUU WA SHULE.

APPENDIX /KIAMBATA (A)

.....
.....
.....

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ITONA,
SLP 414,
MAFINGA.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITONA
MWANAFUNZI.....
KIDATO CHA _____MWAKA_____

1.Mimi ..... Mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, ninakiri kua nimeyaelewa maelezo yote (joining instruction) yaliyotolewa.
2. Ninakubali mwanangu aendelee na masomo, na nitatekeleza yote yale yanayonihusu kwa wakati wake, kama ilivyoagizwa katika maelezo ya kujiunga na shule hii.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidi Kufuatilia/kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapo shuleni.

JINA LA MZAZI/MLEZI.....
SAHIHI YAKE.....
Namba ya simu.....

Mimi.....ninakubali kwa hiari yangu kujiunga na shule hii, naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kuwa na nidhamu, kusoma kwa bidii, na kuwa mfano wakuigwa kwa wanafunzi wenzangu ili nifikie malengo yangu ya kujiunga na shule hii.

JINA LA MWANAFUNZI.....
SAHIHI.....

MAELEZO MENGINE MUHIMU KUZINGATIA

1. Kila mzazi/mlezi na mwanafunzi kujaza **kiambata A** na kukileta siku inapofungua shule
2. Mzazi/mlezi **amlete mtoto kwa wakati uliopangwa** hata kama hajakamilisha mahitaji ataendelea kumkamilishia wakati mtoto anaendelea na masomo.
3. Kila mwanafunzi analazimika kutii na kuheshimu na kujua wimbo wa shule,wimbo wa Taifa,Tanzania Tanzania nakupenda, na Tazama Ramani
4. Cheti cha kuzaliwa(kivuli chake aje nacho)

APPENDIX/KIAMBATA (B):

JINA LA MWANAFUNZI.....
SAHIHI.....

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI ITONA
S.L.P 414 MAFINGA.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE AMBAZO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUZIFUATA

A. SHERIA

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

2. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya popote, wakati wowote na kwa mtu yeyote .

3. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanya kazi wote walioko shuleni kama walezi wake.

4. Mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na kusaidiana na wenzake katika kazi na masomo .

5. Mwanafunzi anatakiwa kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

6. Mwanafunzi HARUHUSIWI kufanya mambo yafuatayo;-
    1. Kuvuta sigara,bangi.
    2. Kutumia madawa ya kulevya.
    3. Kufuga kucha wala kua na nywele zisizo na utaratibu.
    4. Kupaka rangi kwenye kucha,midomo
    5. Kufuga ndevu.
    6. Kuvaa mavazi yasiyokuwa na heshima.
    7. Kugombana.
    8. Kuchelewa.

B. MAHUDHURIO

i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa

ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria/kufanya kazi zote za mikono

iii. Mwanafunzi anatakiwa kufanya mambo yafuatayo
    (a) Kuandika nukuu zote za masomo (lesson notes)
    (b) Kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu
    (c) Kutunza madaftari yake vizuri

iv. Mwanafunzi anatakiwa kuja muda uliopangwa, yaani **KUWAHI SHULENI KWENYE VIPINDI DARASANI**

v. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi kwenye shughuli zote.

vi. Mwanafunzi anatakiwa kukimbia mara asikiapo wito wa kengele au anapoitwa na mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri.

C.UVAAJI WA SARE ZA SHULE

I. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wa kuwa wote awapo shuleni.

II. Anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa,

(a) Masomo darasani.
(b) Anapotoka nje ya shule kwa shuguli za kishule
(c) Mhadhara wa shule
(d) Anapokwenda hospitali
(e) Kwenye maandamano

III. Anatakiwa kuhakikisha kuwa sare yake ni safi wakati wote

D.MIPAKA

I.Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu

II. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo;-

(a) Vilabu vya pombe
(b) Baa
(c) Nyumba za kulala wageni
(d) Majumba ya starehe
(e) Nyumba za walimu zisiwe za mazoea kwa mwanafunzi, epuka

E.Makosa ambayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja

1. Wizi.
2.Uasherati na ushoga.
3. Ulevi/Uvutaji bangi/Madawa ya kulevya.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupiga/kupigana.
6. Kuharibu mali ya umma.
7.Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9.Kupata mimba,au kusababisha Mimba.
10.Kutoa mimba,au kusababisha kutoa mimba.
11. Kupanga mikutano ya kuvuruga amani shuleni.
12. Kugoma adhabu kwa makusudi.
13. Matusi kwa kauli au maandishi ,luga ya dharau,makelel,ugomvi,ni marufuku.
14.Uzinzi, urafiki wa kimapenzi, ubakaji unyanyasaji wa kijinsia,utoro,kiburi ni maruf
15. Kuwa na simu ya mkononi

.....

D.E.MLOWE
MKUU WA SHULE

APPENDIX/KIAMBATA(C) :

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITONA
S.L.P 414
MAFINGA.

DAKTARI .....
HOSPITALI YA .....
S.L.P .....

FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI.

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake, na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa shuleni kuanza masomo ya kidato cha kwanza-2021.

.....
D.E.MLOWE
MKUU WA SHULE

.....

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITONA,
S.L.P 414,
MAFINGA
TAREHE.....

YAH: MWANAFUNZI.....
UMRI.....

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Blood comment (red & white).....
2. Urine.....
3. Stool.....
4. Pregnancy test.....
5. BP test.....
6. Ear test.....
7. Eye test.....
8. Spleen.....
9. Additional information,any other physical,hereditary or infectious diseases.....
   .....

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ..... ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari kwa sababu:

.....
.....

JINA LA DAKTARI .....SAHIHI.....

CHEO/WADHIFA.....TAREHE.....MUHURI